
# MUNGU ATAZAMAYE MOYO

Mafunzo ya Watoto
~Darasa la Saba



Mch Denis & Devis Julius

# MUNGU ATAZAMAYE MOYO

Huu ni mwendelezo wa mafunzo ya watoto, na hili ni darasa la nane(8), Mafunzo haya ni mwongozo kwa mwalimu wa watoto kuwafundisha kivitendo, juu ya kuuelewa wokovu kwa kina, na jinsi ya kuishi maisha ya Imani. Ikiwa huu ndio mara yako ya kwanza kukutana na madarasa haya, ni vema ukapata madarasa ya nyuma. Hivyo kuwasiliana nasi kwa namba uzionazo mwishoni mwa chapisho hili.

Ni wajibu wetu sote kuwainua na kuwalea watoto katika misingi sahihi ya imani katika kizazi hiki kinachoharibika kwa kasi.

Madarasa haya ni kwa watoto wasiozidi umri wa miaka kumi na mbili (12), Ikumbukwe kuwa kuwafundisha watoto mpaka kuelewa ipasavyo kunahitaji moyo wa upendo kwao, uvumilivu,kuwaombea lakini pia kuwafundisha zaidi kwa mifano na vitendo na picha zaidi ya maneno tu, kwasababu uelewa wa watoto bado

ni wa kuona zaidi sio wa kufikiri sana kama mtu mzima. Ndio maana akienda shule ili kuelewa somo la hisabati mtoto ataletewa vijiti na kuvihesabu ndipo aweze kutoa jibu. Lakini hesabu sio vijiti, isipokuwa vijiti humsaidia kufikia uelewa wake.

Vivyo hivyo katika kuwafundisha watoto mambo ya rohoni, ni vema zaidi ukatumia njia ya hadithi, picha, nyimbo, maigizo. Ili vimsaidie kukumbuka ujumbe ambao anatakuwa kuupokea katika madarasa yako, hilo ni muhimu sana, Na hatimaye ataelewa vema kwa neema za Mungu.

**Kuchaguliwa kwa Daudi Kuwa Mfalme**

Kundi la Umri: Miaka 6–12

Mada: Mungu Huutazama Moyo

Vifungu mama: 1 Samweli 16:1–13

1 Samweli 16:1-13

*[1]BWANA akamwambia Samweli, Hata lini utamlilia Sauli, ikiwa mimi nimemkataa asiwamiliki Israeli?*

*Ijaze pembe yako mafuta, uende, nami nitakupeleka kwa Yese, Mbethlehemi; maana nimejipatia mfalme katika wanawe.*

*[2]Samweli akasema, Nawezaje kwenda? Sauli akipata habari, ataniua. Basi BWANA akasema, Chukua ndama pamoja nawe, ukaseme, Nimekuja ili kumtolea BWANA dhabihu.*

*[3]Ukamwite Yese aje kwenye dhabihu, nami nitakuonyesha utakayotenda; nawe utamtia mafuta yule nitakayemtaja kwako.*

*[4]Samweli akafanya hayo aliyosema BWANA, akaenda Bethlehemu. Wakaja wazee wa mji kumlaki, wakitetemeka, nao wakasema, Je! Umekuja kwa amani?*

*[5]Naye akasema, Naam, kwa amani; nimekuja kumtolea BWANA dhabihu; jitakaseni; njoni pamoja nami kwenye dhabihu. Akawatakasa Yese na wanawe, akawaita kwenye dhabihu.*

*[6]Ikawa walipokuja, alimtazama Eliabu, akasema, Yakini masihi wa BWANA yupo hapa mbele zake.*

*[7]Lakini BWANA akamwambia Samweli, Usimtazame uso wake, wala urefu wa kimo chake; kwa maana mimi*

*nimemkataa. BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali BWANA huutazama moyo.*

*[8]Ndipo Yese akamwita Abinadabu, akampitisha mbele ya Samweli. Naye akasema, BWANA hakumchagua huyu.*

*[9]Ndipo Yese akampitisha Shama. Naye akasema, wala BWANA hakumchagua huyu.*

*[10]Yese akawapitisha wanawe saba mbele ya Samweli. Samweli akamwambia Yese, BWANA hakuwachagua hawa.*

*[11]Kisha Samweli akamwambia Yese, Watoto wako wote wapo hapa? Naye akasema, Amesalia mdogo wao, na tazama, anawachunga kondoo. Basi Samweli akamwambia Yese, Tuma watu, wamlete; kwa sababu hatutaketi hata atakapokuja huku.*

*[12]Basi akatuma mtu, naye akamleta kwao. Naye alikuwa mwekundu, mwenye macho mazuri, na umbo lake lilikuwa la kupendeza. BWANA akasema, Ondoka, umtie mafuta; maana huyu ndiye.*

*[13]Ndipo Samweli akaitwaa pembe yenye mafuta, akamtia mafuta kati ya ndugu zake; na roho ya*

*BWANA ikamjilia Daudi kwa nguvu tangu siku ile. Basi Samweli akaondoka, akaenda zake Rama.*

**Kifungu cha Kukariri:**

*1 Samweli 16:7 – "..BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali BWANA huutazama moyo."*

**Lengo Kuu:**
Watoto wajifunze kuwa Mungu hachagui watu kwa sababu ya sifa za nje au kwa mwonekano wao, bali kwa moyo umpendezao.

## UTANGULIZI


Waulize watoto maswali kwa vitendo:

Waweke watoto wawili mbele, mmoja mdogo na mwingine mkubwa, kisha waulize watoto wengine, je! kati ya hawa wawili, ni nani anayeonekana mwenye nguvu kuliko mwenzake? Ni nani anaweza kuchaguliwa kuwa kiongozi? Watakujibu.

Au tumia picha ya watu wawili, mmoja ana nguvu mrefu na msuli mikubwa, mwingine mdogo, dhaifu ana sura ya upole, kisha waulize watoto maswali yale yale ni nani anayeonekana kuwa na nguvu, ni nani anayestahili kuwa askari?

Watakujibu

Chukua mfano huu wa picha. Ukusaidie kuwafundisha watoto.



Ukweli ni kwamba watoto wengi watasema, yule mrefu, mwenye nguvu mwenye misuli mikubwa ndiye kiongozi.

Waeleze kuwa mara nyingi wanadamu wanahukumu kwa kutazama mwonekano wa nje, lakini kwa Mungu ni

tofauti yeye anatazama mtu moyo

Simulizi ya Daudi kuteuliwa mfalme..

Mwl: Simulia kwa utaratibu na misisimko kwa lugha rahisi habari ya Samweli alivyotumwa na Mungu kwenda katika nyumba ya Yese kumteuwa mfalme:

- Mungu alimtuma Samweli kwa Yese kumchagua mfalme mpya.
- Samweli alimwona mwanawe wa kwanza aliyeitwa Eliabu na kudhani ndiye.
- Mungu akasema: “Si huyu.”
- Wana wengine wote wakapita, Mungu hakuwachagua.
- Daudi, aliyekuwa akichunga kondoo, akaitwa.
- Mungu akasema: “Huyu ndiye.”
- Samweli akamtia mafuta Daudi.

**Igizo**

Tengeneza izigo kwa kuwapa watoto nafasi ya kuwa Samweli, Yese, Daudi na wale ndugu saba wa Daudi. Jinsi Samweli alivyoingia kwenye nyumba ya Yese, mpaka kumchagua Daudi.

Hilo litawasaidia hadithi hiyo kudumu kwa muda mrefu moyoni mwao.

**Kifungu cha Kukariri watoto**.

1 Samweli 16:7

*Wafundishe kurejea hiki kifungu mara kwa mara hadi wote wakikariri vema.*

## **Mafundisho Makuu**.

Mungu huangalia moyo. Anaweza kumtumia mtu yeyote, kumwongoza yoyote, haijalishi ni mtoto kama wewe, Mungu anaweza kukutumia kuwaponya, au kuwafundisha au kuwasaidia watu wengi endapo tu utazingatia kuwa na moyo ambao anaompendeza yeye

Moyo unaompendeza Mungu ni upi?

1. **Utii**

Utii kwa wazazi, maalumu wako wa kanisani pamoja na waalimu wako wa shuleni.

**2) Uaminifu**

Unapoagizwa kufanya kitu hata kama ni kidogo, kifanye bila kulegea, kupunguza, au kuiba, unapokuwa

mwaminifu nyumbani, Mungu atakuamini pia kukutumia wewe kama Daudi.

**3) Upendo**

Mungu ni upendo, wafundishe mtoto anapoonyesha upendo kwa Mungu na wenzake, anajiandaa kuwa mpenzi wa Mungu.. Kupenda ni pamoja na kuwaombea wenzake, kuwahubiria, kuwasaidia, kuepuka kupigana, kukemea uovu,

**4) Sala.**

Wafundishe kuwa Mungu anazungumza nasi kwa njia ya sala, mtu ambaye anapenda maombi, anaongeza daraja lake la kupendwa na Mungu. Hivyo wapende sala lakini pia wakisikia ratiba za maombi kanisani au nyumbani basi wasizikwepe

**5) Imani**

Wafundishe Neno la Mungu linasema..pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu(Waebrania 11:6)

Wafundishe kuamini kuwa Mungu yupo na wao, anasikia maombi yao, ni mweza yote, ndiye anayewasimamie katika mambo yao yote, wafundishe kuwa mwanadamu anayemtegemea Mungu katika

mambo yake yote, anajiweka katika daraja zuri la kuchaguliwa na Mungu, kama vile Daudi.

Yeye alipofika kwa mfalme, kwa Imani alimwambia Sauli mimi nitamuua yule Goliathi, kwasababu Mungu yule aliyekuwa nami nyikani, mpaka nikawaua Dubu na Simba atakuwa nami hata mbele ya huyu Goliathi, .(1 Samweli 17:34–37)

Hiyo pia ilikuwa sababu ya Mungu kupendezwa na Daudi.

## MASWALI YA MAJADILIANO

Ni vema mara baada ya hadithi hizo ukawauliza maswali, kupima uelewa wao, kisha wajifunza kwa njia ya majadiliano.

Waulize maswali haya;

- Kwa nini Samweli alidhani Eliabu ndiye angekuwa mfalme?
- Daudi alikuwa wapi?
- Mungu huangalia nini?
- Unawezaje kuwa na moyo unaompendeza Mungu?

## Vitendo vya kufanya Kila Siku

Wawapo Nyumbani: Watii wazazi, Waseme ukweli, Wasaidie kazi.
Shuleni: Waheshimu walimu, Wasidanganye, wapende wenzao.

**Zoezi la wiki:**

Fanya jambo moja litakaloonyesha moyo unaompendeza Mungu.

**Funzo kwa vitendo zaidi**

Mpe kila mtoto karatasi ya umbo la moyo.
Ndani ya moyo aandike: Upendo, Utii, Ukweli, Huruma, Sala.
Nje ya moyo achore vitu vya nje kama mavazi au nywele.
Eleza kuwa Mungu huona kilicho ndani ya moyo.

**Wimbo:**

Wafundishe wimbo wa wokovu au pambio, lenye maudhui ya moyo safi umpendezao Mungu.

Tenzi: No. 55 - Nipe moyo wenye sifa.




**Sala ya mwisho**.

"Baba yetu uliyembingubi asante kwa mfano wa Daudi. Tusaidie kuwa na mioyo inayokupendeza, tuwe waaminifu, watiifu na wenye upendo na Imani. Tutumie angali tukiwa ni watoto. Ni Katika jina la Yesu, tumeomba na kushukuru  Amina."

**Hitimisho:**

"Mungu anaweza kumchagua mtu mdogo mwenye moyo mkubwa."

**Mawasiliano:**

Mch. Denis & Devis Julius

Tel: +255 693 036 618 / +255 789 001 312

Kanisa la Nuru ya Upendo wa Kristo